*MERCHANT SHIPPING NOTICE*
*MSN 1410*

**Rejeo 2/2022**

***Tangazo hili linatolewa kwa Wamiliki wa Vyombo Vidogo vya Majini, Waendesha vyombo, Wamiliki wa Bandari na Mialo, na Wananchi kwa Ujumla***

# HATUA ZA KUBORESHA USALAMA NA ADHABU KWA MAKOSA YA VYOMBO VIDOGO MAJINI

***Tangazo hili lisomwe pamoja na 'The Merchant Shipping (Small ships, local cargo ship safety, small ship safety, surveys and inspections for vessels engaged in local and coastal voyages, Inland waters) (Amendments) Regulations, 2012' na Tangazo MSN 0908 Maelekezo Juu ya Usalama wa Vyombo Vidogo vya Majini na Hatua za Kuchukua Kuepusha Ajali za Vyombo Hivyo***

## 1.0 Hatua za Kuboresha Usalama

1.1 Ni muhimu kwa wamiliki na waendesha vyombo vidogo, wafanyakazi wa vyombo vya mizigo na uvuvi na abiria wa vyombo vya abiria wa usafiri majini, kuzingatia kwamba **Chombo salama** ni kile kinachoweza kukabili hatari za majini za kawaida; mazingira mazuri kuhusu afya, na kuhakikisha usalama na ustawi wa maisha ni nzuri. Usalama wa chombo kiwapo majini inajumuisha mambo yafuatayo:

(a) Umadhubuti wa chombo chenyewe;
(b) Vifaa vya chombo kuwa katika hali nzuri ya kufanya kazi;
(c) Chombo kuwa na wafanyakazi wa kutosha, wenye ujuzi unaostahili na wenye afya njema;
(d) Mashine au mitambo mingine ya chombo kuwa nzima na kufaa kwa safari iliyokusudiwa; na
(e) Chombo kubeba abiria au mizigo kulingana na uwezo wake na mizigo kupakiwa inavyostahili.

1.2 Wamiliki na waendesha vyombo vidogo wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo ili kudumisha usalama:

1.2.1 Alama inayoonesha kina cha mwisho kilichoruhusiwa na Mkaguzi wa Mamlaka husika (TASAC) kwa chombo kidogo cha abiria , uvuvi au mizigo kudidimia majini wakati kinaelea vizuri majini (loading mark), iwakilishwe kwa kibati maalum kilichobandikwa katikati ya chombo, pande zote mbili nje;

1.2.2 Kibati kilichotajwa kwenye kifungu 1.2.1, kitakuwa na urefu wa 300mm na upana wa 25mm na kubandikwa bila kutoka (permanent);

1.2.3 Chombo kidogo cha mizigo au abiria hakiruhusiwi kuanza safari kama maji yatakuwa yamefunika kibati hicho;

1.2.4 Chombo kidogo chochote hakiruhusiwi kuanza safari kama hakina idadi ya majaketi ya kujiokolea (lifejackets) inayolingana na watu walioruhusiwa na mkaguzi wa TASAC kubebwa na chombo hicho;

1.2.5 Ni muhimu watu kuvaa majaketi ya kijiokolea wakati zote wawapo ndani ya boti ya majini , kuvaliwa kabla ya chombo kuanza safari;

1.2.6 Chombo cha abiria hakiruhusiwi kubeba mizigo, isipokua mizigo ya abiria ya mikononi;

*1.2.7* Idadi ya abiria ambao chombo kidogo kimeruhusiwa kubeba na mkaguzi wa TASAC iandikwe kwa maandishi makubwa ubavuni nje, pande zote mbili mbele mwa chombo husika kama ifuatavyo:
***'Boti hii inaruhusiwa kubeba watu…'***

1.2.8 Chombo kidogo ambacho hakikusajiliwa na TASAC kubeba abiria hakiruhusiwi kubeba abiria, labda kwa kibali maalum cha muda mfupi;

1.2.9 Vyombo vidogo vya abiria na mizigo haviruhusiwi kutoka mwaloni kama hali ya hewa sio rafiki na vilevile haviruhusiwa kufanya safari za usiku;

1.2.10 Vyombo vidogo vya abiria haviruhusiwi kuchanganya abiria na mizigo, mifugo na vitu vya mlipuko;

1.2.11 Vyombo ambavyo haviendeshwi kwa injini haviruhusiwi kubeba abiria;

1.2.12 Abiria au mfanyakazi mwenye dalili ya kilevi chochote haruhusiwi kusafiri na chombo chochote cha majini;

1.2.13 Chombo kidogo cha mizigo hakiruhusiwi kubeba watu wanaozidi idadi iliyoainishwa kwenye cheti chake cha ubora; na

1.2.10 Uzito (katika tani) ambao chombo kidogo cha mizigo kimeruhusiwa kubeba na mkaguzi wa TASAC iandikwe kwa maandishi makubwa ubavuni nje, pande zote mbili mbele mwa chombo husika kama ifuatavyo: ***'Boti hii inaruhusiwa kubeba tani…'***

## 2.0 Adhabu kwa Makosa

Makosa na adhabu ya vyombo vidogo vya majini ili kuzuia ajali za majini na kulinda maisha ya watu na mali zao yameainishwa katika jedwali lililoambatishwa.

Utekelezaji wa tangazo hili utawezesha waendesha vyombo kutoa huduma bora ya usafiri majini isiyo na usumbufu na inayowajali watumiaji.

**Taarifa Zaidi Wasiliana na:**
Msajili
Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)
Ghorofa ya 8 PSSSF TOWER, Ohio Street / Garden Avenue
S. L. P 989
Dar es Salaam
Tanzania
Simu: +255 22 2127314
Nukushi: +255 22 2127313
Barua pepe: **dg@tasac.go.tz**, **infor@tasac.go.tz**
**Tovuti:** **www.tasac.go.tz**

***Jedwali***

**Adhabu kwa Makosa ya Vyombo Vidogo**

| Na. | Aina ya Kosa | Adhabu ya kosa/Faini | Mhusika wa kulipa |
|---|---|---|---|
| 1 | Kutumia chombo kidogo majini ambacho hakijawekewa alama ya ukomo wa kupakia (loading mark) au chombo kidogo kuanza safari wakati alama ya ukomo imezama majini | Faini ya shilingi 500,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Mmiliki na nahodha wa chombo kila mmoja |
| 2 | Kutumia chombo kidogo cha majini ambacho hakijakaguliwa na kupewa cheti cha ubora | Faini ya shilingi 500,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Mmiliki na nahodha wa chombo kila mmoja |
| 3 | Kupeleka chombo cha abiria au mizigo majini bila kujaza fomu za ruhusa ya kutoka bandarini au bila kuhakikisha taarifa za chombo chake zimeingizwa kwenye daftari maalum na msimamizi wa mwalo husika | Faini ya shilingi 300,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha wa chombo |
| 4 | Kutumia chombo kidogo ambacho hakina vifaa vya kutosha vya kuokolea maisha | Faini ya shilingi 300,000/= | Mmiliki na Nahodha wa chombo kila mmoja |
| 5 | Chombo kidogo cha abiria au mizigo kuanza safari yake usiku | Faini ya shilingi 300,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha na Mmiliki wa chombo kila mmoja |
| 6 | Chombo kidogo kupakia abiria kuzidi uwezo wake kama | Faini ya shilingi 500,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha wa chombo na Mmiliki wa chombo kila mmoja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ilivyoainishwa katika cheti cha ubora | | |
| 7 | Chombo kidogo cha abiria au mizigo kuanza safari kutokea bandari au mwalo usio rasmi | Faini ya shilingi 300,000/= au kifungo miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha wa chombo |
| 8 | Chombo kidogo cha mizigo kubeba abiria au chombo kidogo kisichoendeshwa kwa mashine (injini) kubeba abiria | Faini ya shilingi 500,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Mmiliki wa chombo na Nahodha kila mmoja |
| 9 | Kupeleka chombo nje ya eneo salama kama linavyooneshwa katika cheti cha ubora | Faini ya shilingi 100,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha wa chombo |
| 10 | Kukaidi maagizo halali ya yaliotolewa na kutangazwa na Shirika kwa lengo la kuboresha usalama majini | Faini ya shilingi 300,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Mmiliki wa chombo na Nahodha kila mmoja |
| 11 | Chombo kidogo kufanya safari nje ya eneo la maji lilioainishwa kwenye cheti chake cha ubora | Faini ya shilingi 500,000/= au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote faini na kifungo | Nahodha wa chombo |

**Zingatia:**

**1:** **Makosa na adhabu zake katika jedwali hili ni kwa ajili ya wamiliki na waendesha Vyombo Vidogo Majini**

**2.** **Utekelezaji unaanza mara moja.**